

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 23222761-5
Fax No. +255 026 2322624
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imepanga kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022, The written Laws (Financial Provisions) (Amendment) Bill 2022. kwa mujibu wa Kanuni ya 97(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mkutano wa kupokea na kusikiliza maoni ya wadau (**Public Hearing**) utafanyika siku ya **Jumane tarehe 20, Septemba 2022 saa 4:00 asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa**, Ofisi ya Bunge Jijini Dodoma.

Kamati inawaalika watu wote wenye maoni kuhusu Muswada huo kufika na kuwasilisha maoni yao kabla haujapelekwa katika hatua nyingine.

Vilevile itapokea maoni kwa njia ya posta au Barua pepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,
Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole,
S.L.P. 941,
41105 DODOMA.

Baruapepe: cna@bunge.go.tz na kamati@bunge.go.tz

Muswada huo pia unaweza kupakuliwa katika tovuti ya Bunge, www.bunge.go.tz. Aidha, unashauriwa kuwasilisha jina lako kupitia barua pepe tajwa endapo utapenda kuwasilisha maoni yako kwa kuzungumza kwa ajili ya hatua zaidi.

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
DODOMA.

19 Septemba, 2022.